

حقائق عن الخميني

UKWELI KUHUSU

KHOMEINI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Khomeini ni mtu wa uwazi katika kauli zake, na ni muwazi katika chuki zake, na muwazi katika uadui wake, na muwazi katika itikadi zake, wala hamuachi msomaji wake kwenye shaka zozote zile ili ajijengee sura ya wazi kabisa kuhusiana nae na itikadi na rai zake, ambazo amezikusanya kwenye vitabu na khotuba zake kwa uwazi kabisa

Katika kurasa hizi tutajaribu kutambua ukweli juu ya Khomeini, na kuweka bayana juu ya uhalisia wake kwani wafuasi wake mara nyingi wamejaribu kuuficha ukweli wake kinyume na msimamo wake yeye mwenyewe, wamekwenda mbali hata kumfikia kumtukuza, na kumfanya kuwa ni ufunguo pekee wa maarifa ya itikadi ya kiislam. Kwa maana hii ndiyo tumeona umuhimu kurejea kwa Khomeini mwenyewe ili kuujua ukweli wake hasa, mbali na yaliyosemwa kuhusiana nae, na hapana shaka kwamba vitabu vyake vingi vinatosheleza kumuelezea yeye ni nani, hivyo tuliona umuhimu wa kuvipitia na tumetoka na haya:

1- Alkhomeiny anasema: Sisi hatumuabudu Mungu ambae anajenga jengo kubwa la uungu na uadilifu na dini kisha analiharibu kwa mikono yake.

"Sisi tuna muabudu Mungu ambae tunajua kwamba matendo yake yana zingatia msingi wa akili, wala hafanyi matendo yanayo kwenda kinyume na akili, na sio Mungu ambae anajenga jengo kubwa la uungu na uadilifu na dini kisha analiharibu kwa mikono yake, na anampa uongozi Yaziid na Muawiyya na Othman na mfano wao miongoni mwa muhajirin, wala haelezei kinacho takiwa kwa watu milele baada ya Mtume ﷺ, ili asipate kusaidia katika kujenga jengo la dhulma na kudhulumiana".¹

2- Alkhomeiny anakubali Uwepo wa kubadilishwa kwa Qur ani tukufu

“Anaeweza kuipokea Quran hii pekee ni Mtukufu na mbora wa mawalii Ally bin Abi Talib, na hakuna wengine wowote wale wanaoweza kuchukua uhakika huu ila kwa kushuka kutoka daraja ya ghaibu hadi kufikia daraja ya shahada (kudhihiri) na kupitia kwa malaika na kwa kuvalishwa maneno na herufi za kidunia, na hii ni moja ya maana ya tahriif (kubadilishwa) ambako kumejitokeza katika vitabu vyote vya Mbinguni ikiwemo na Qur-an tukufu na aya zake zote, vyote vimewekwa katika mikono ya waja baada ya mabadiliko mbalimbali kwa mujibu wa uteremkaji wake na hatua zilizo pitia, tokea pale vilipokua ni

¹ Iktishaf al-asrari, 116-117

majina tu hadi kudhihiri kwake na kwenda kwa malaika wa mwisho. Na idadi ya hatua za tahriif zinaendana na idadi ya matumbo ya Qur-ani, zinafanana kama vinavo fanana viatu".¹

3- Alkhomeiny anafanya ilhadi katika aya za Allah na anatafsiri kauli ya Allah isemayo:

﴿يَدِيرُ الْأَمْرَ فُصِّلَ الْآيَاتُ لَكُمْ لِقَاءَ رَبِّكُمْ تُرَوُّونَ﴾ [الرعد: ٢]

kasema " ربكم " yaani Imamu, kasema: Yaani rabbukum ambae ni Imamu. Tazama vipi maneno ya Allah yalivyo bora na hekima.²

(Angalizo: Angalia vipi Khomeini anavyokwenda kinyume na maneno yake Allah na kubadilisha maana yake, na tazama vipi hali ya kuchupa mipaka na shirki jinsi zilivyoshikana na maneno yake).

4- Alkhomeiny anasema: Mtume ﷺ hakupata tawfiq katika daawa yake:

"Kadhia ya kufichikana kwa Imamu ndio kadhia muhimu inayo tubainishia mambo mbali mbali, katika hayo ni kwamba haiwezekani kwa mtu yeyote kutimiza amali kubwa kama hii ya kujenga uadilifu uliokamilika ulimwenguni kote na kwa watu wote, isipokuwa Mahdy Almuntadhar (sa) ambaye Allah Mtukufu amemueka akiba kwa ajili ya viumbe. Kila Mtume alikuja kwa lengo la kusimamisha uadilifu, na lengo lake lilikuwa kwa ulimwengu mzimza lakini hakupata mafanikio. Na hata Mtume wa mwisho Muhammad ﷺ na yeye pia alikuja kwa ajili ya kuwatengeneza watu na kuwapamba vizuri na kutekeleza uadilifu lakini na yeye pia hakufanikiwa, na kwamba atakae fanikiwa kikamilifu na kutimiza uadilifu katika pembe zote za ulimwengu ni Mahdy peke yake"³

“Angalizo: Jee kuko kumkashifu na kumvunjia heshima Mtume ﷺ zaidi ya hivi? jee yako maneno ya maadui wa uislam zaidi ya maneno haya?”

5- Alkhomeiny anamtuhumu Mtume kwa kuogopa kufikisha amri ya Allah kwa khofu ya kuja kubadilishwa Qur-ani:

"Kwa mkusanyiko wa dalili hizi na mapokezi ya hadithi inatubainikia kwamba Mtume alikua anaogopa kulingania Uimamu, na atakae rejea katika vitabu vya tarekhe na historia atajua kuwa Mtume (saw) alikua na haki ya kuogopa, lakini Allah akamuamrisha afikishe na akamuahidi kumlinda".⁴

"Tumethibitisha mwanzo wa mazungumzo haya kwamba Mtume alijizuilia kuzungumzia uimam katika Qur-ani kwa kuogopa kuwa Qur-ani isije ikakumbwa na tahriif baadae"⁵

Angalizo “Khomeini hapa amepindukia mipaka ya kutohe-shimu, hakutoshelezeka kwa kumsifu Mtume ﷺ kuwa ni mwoga,

¹ Al qur-ani: babu maarifatullah, 50.

² Misbahu lhidaya ilaa lkhilafati walwilaya, 150.

³ Mukhtarat min ahadithi wakhutabati Al-imam Al-khomeinyi, 2/43

⁴ Kashfi al-asrari, 150

⁵ Kashfu al-asrari, 149

bali amemtengezea udhuru ambao haupo katika akili ya muislam achilia mnafiki, tuchukulie kwamba Mtume ﷺ alikuwa mwoga jambo ambalo asili halipo kuwa aogope utiifu kwa Allah, Jee itakuwa sababu ya khofu yake ni kuharibiwa Quran, Jee amesahau Mtume ﷺ ahadi ya Allah kwake ya kukilinda kitabu chake au amekuwa na shaka na hilo? Hapana, hilo halipo kwake. Lakini ni wazi kwamba Khomeiny yuko tayari kwa vyovyote kumtia dosari Allah na Mtume wake kwa ajili ya kutumikia madhehebu yake, ni kiasi gani anaukaribia moto?”

6- Alkhomeiny anamtuhumu Mtume ﷺ kwa kushindwa kufikisha ujumbe:

"Ni wazi kwamba Mtume kama angefikisha ujumbe wa uimamu kama alivyo amrisha na Allah na akafanya jitihada katika jambo hilo kusingetokea tofauti, mapigano na vita baina ya nchi za Kiislamu na kusingelikuwa na tofauti katika misingi ya dini (usuuli diin) na furui zake (matawi yake)"¹

"Kwa hakika Manabii wote walikuja kwa lengo la kuweka misingi ya uadilifu ulimwenguni lakini hawakufanikiwa, hata Mtume Muhammad ﷺ ambae ni Mtume wa mwisho nae pia alikuja kuwatengeneza waja na kutandika uadilifu pia na yeye hakufanikiwa katika hilo"²

Angalizo: “Vipi kwa mwanachuoni na marjii anaedai uislam, amsifu Mtume wa uislam ﷺ kwamba ameshindwa kufikisha ujumbe kama vile alivyotakiwa na Allah, na kama siyo hivyo atakuwa amefanya kwa matakwa ya nani? Khomeini hajalijibu suala hili, mwanzo amemtuhumu kwa woga, na hapa anamtuhumu kushindwa kufikisha ujumbe, ni dini gani ya mtu huyu na ni imani gani anayodai?, na kwa kauli kama hii ndio wanachuoni wakasema ni kauli ya mtu mzandiki na siyo kauli ya mwanachuoni muislam “

7- Alkhomeiny anasema: Mtume ﷺ hakuweza kuipata serikali aliyoikusudia:

"Ninasikitishwa na mambo mawili, moja lina sikitisha zaidi kuliko jengine. La kwanza ni kwamba tokea mwanzo wa uislam na utume na zama zilizofuata, hawakuachia kudhihiri serikali inayotakiwa na uislam. Katika zama za Mtume ﷺ kwa sababu ya matatizo mbalimbali ya kivita na upinzani haikupatikana serikali kama alivyoitaka Mtume ﷺ "³

8- Alkhomeiny anathibitisha uwepo wa Mtume mwengine anaepokea wahyi, na miongoni mwa wahyi huo ni kuhusu Mapinduzi yake:

"Fatma Zahraa baada ya kufa kwa baba yake alikuwa na

¹ Kashfu al-asrari, 155

² Haya yamo katika hotuba aliyoitowa kwenye mnasaba wa kuzaliwa imamu Al-mahad almaadum, tazama kitabu cha Nahaj khomeiny, uk 46

³ Mukhtaraat min ahadithi wa khutabat al-imam al-khomeiny, 2/520

huzuni kubwa na majonzi siku sabiini na tano, na Jibril alikuwa anamjia kumliwaza na kumjulisha mambo ambayo yatatokea siku za mbele. Na niwazi kwa mujibu wa riwaya hii kwamba Jibril katika kipindi hicho cha siku sabiini na tano alikuwa anakuja mara kwa mara kwa Fatma, wala sidhani kuwa riwaya mfano wa hii imewahi kutokea kwa mtu yeyote ukiacha mbali wale Manabii wakubwa, na Imam Aliy alikua anaandika mambo haya aliyokua analetewa Fatma na Jibril!, na inawezekana kwamba kadhia za Iran ni katika jumla ya mambo aliyoletewa".¹

Angalizo: (Sidhanii kwamba kauli yake hii inahitajia maoni zaidi lakini tunamshukuru Allah kwa neema ya akili na fahamu na tunamuomba asiturejeshe katika umri wa chini).

9- Khomeini anathibitisha kuwepo msahafu mwengine zaidi ya Quran.

"Jibril alikuwa baada ya kufariki Mtume ﷺ akija kwa Fatimah na habari za ghaibu, na Amiri al-muumina Ally alikuwa akiziandika na huu ndio msahafu wa Faatimah"²

10- Alkhomeiny anadai kwamba Aliy ndie msimamizi wa kila nafsi na inacho kichuma:

"Hakika yeye alayhi salam ndie mwenye utawala usio mipaka... kwani yeye alayhi salam kwa utawala wake waujumla huisimamia kila nafsi na ilicho kichuma kwa ujumla, na kila kitu kiko pamoja na usimamizi wa kivuli cha uungu "³

11- Alkhomeiny anasema: Aliy angedhihiri kabla ya Mtume angeidhihirisha sharia na angekua Mtume:

"Kama Aliy (as) angedhihiri kabla ya Mtume angelidhihirisha sharia kama alivoidhihirisha Mtume ﷺ na angekuwa Nabii aliye tumwa kwa watu, kwa jinsi walivyoungana kiroho na darja zinazo onekana na zisizo onekana".⁴

12- Alkhomeiny anasema: Aliy ni kila kitu kwetu na anachukua nafasi ya mwanzo katika mambo yetu yote ya kiutu na wajibu wetu ni kumfuata:

"Ni lazima mambo yenu yote yafuate riadha na malezi ya kiroho. Muangalieni Aliy (as) popote tunapo kwenda tunaliona jina lake! Kwa wanafiqhi tuna sikia kuhusu fiqhi ya Aliy (as), na kwa watu wa zuhdi tunasikia kuhusu zuhdi ya Aliy (as), na kwa watu wa tasawwuf tunasikia kuhusu tasawwuf yake (as), na tunapokwenda kwa watu wa riadha ya kiroho tunawaona wana kariri jina la Aliy (as) na wanaanza riadha yao kwa kutaja jina lake. Aliy huyu ndiye kila kitu kwetu, yeye anachukua nafasi ya

¹ Khutba ya Alkhomeiny kwa mnasaba wa siku ya mwanamke huko Iran tarehe 2/3/1986 na imetangazwa na radio Tehran kwa sauti yake na kunakiliwa na magezeti mbalimbali ya kiarabu

² Kashfu al-asrari, 143

³ Misbahu al-hidaya ila akhilafa walwilaya alkhoayniy, 153

⁴ Misbahu al-hidaya ila akhilafa walwilaya alkhoayniy, 153

mwanzo katika mambo yetu yote ya kiutu, na wajibu wetu sote ni kumfuata. Katika ibada ilikuwa ibada yake iko juu zaidi kuliko ibada za wengine, na katika zuhdi alikua anawashinda watu wote wa zuhdi, na katika viwanja vya vita alikua anawashinda wapiganaji wote, na kwa upande wa nguvu alikua anawashinda wenye nguvu wote, alikua ni mtu wa ajabu alie kusanya sifa tofauti".¹

Angalizo: Maneno haya ni ya mtu asieamini kua Muhammad ni Rasuulullah (Mjumbe wa Allah) kwa namna yeyote atakayodai. Na tunawaambia wenye akili: Jee bado munadai kuthibitishiwa kauli ya "Kapotea Jibril". Khomeiny kaitamka kwa ulimi wake na kuiandika kwa mikono yake.

13- Alkhomeiny anaitakidi kuwa maimamu wana sifa ya kujua kila kitu na kukisimamia:

"Manabii na mawasii (as) wanadaraja kubwa za kiroho zinaitwa roho takatifu na kwa kupitia hali hiyo wana uwezo wa kujua na kusimamia viumbe wote mpaka chembe ndogondogo kabisa".²

14- Alkhomeiny anasema: Hakuna anaeweza kufikia katika darja ya Maimamu, si Malaika alie karibu wala Mtume katika Mitume!

"Katika mambo muhimu ndani ya madhehebu yetu ni kwamba hakuna anaefikia darja za Maimamu si Malaika waliokaribu wala Mtume katika Mitume".³

15- Alkhomeiny anasema: Maimamu wanahudhuria katika vichwa vya watu wanaokata roho!

"Kama tunavyo itakidi sisi na wao wanaitakidi hivyo hivyo na khabari mbalimbali zinazungumza kwamba Amirul Muuminiin (as) anahudhuria katika vichwa vya wanaokata roho ikiwa ni muislamu au kafiri au mnafiki".⁴

Angalizo: Mbali na kuona kwamba maneno haya yanakwenda kinyume na yale yanayotambulika katika dini kwa uyakini, lakini Khomeiny hakutuambia endapo na Mtume anahudhuria na yeye au darja hiyo ni maalum kwa ajili ya Aliy (r.a) tu.

16- Alkhomeiny anasema: Vitabu vya amali vina pelekwa kwa Mahdi wa Shia.

"Tuna uwezo wa kuangalia hali ya vitabu vya amali zetu kabla hazijapelekwa kwa Mola Mtukufu na kabla havija pelekwa kwa swahibu zamaan (sa), kwani vitabu vya amali zetu hupelekwa kwa Imam swahibu zamaan (sa) mara mbili kwa wiki kwa mujibu wa riwaya"⁵

¹ Mukhtarati min ahadithi wa khutabat al-imam al-khomeiny, 1/294

² Al-arbauna hadithi lilkhomeiny, 597

³ Alhukumat al-islamiyah, 93

⁴ Almiadi fy nadhari al-imam alkhomeini, 177

⁵ Almiadi fy nadhari al-imam alkhomeini, 318

17- Alkhomeiny anaona kuwa sikukuu ya kuzaliwa Mahdi ni kubwa zaidi kuliko sikukuu ya kuzaliwa Mtume ﷺ:

"Hakika mazazi ya Imam Mahdi ni sikukuu kubwa kwa waislamu!? na inasadikika kwamba ni kubwa zaidi kuliko mazazi ya Mtume Muhammad ﷺ".

Angalizo: Hii ndio daraja ya Mtume ﷺ katika nafsi ya bingwa wa ulimwengu na muasisi wa mapinduzi ya dunia dhidi ya majeuri na madhalimu. Tunachokisisitiza ni kwamba Khomeiny si mdhaifu wa lugha bali hii ndio itikadi yake anayojifaharisha nayo na kuitangaza kwa watu na anajua yakini kwamba maana ya maneno yake ni kwamba Mahdy ni bora kuliko Mtume ﷺ.

18-Khomeini anawakafirisha Abubakar, na Omar na anawaita kuwa ni wajinga, wapuuzi waongo na wazandiki.

“Sisi hapa hatuna habari yoyote kuhusiana na masheikh wawili, na makosa waliyoyatenda kwenye Quran kwa kuchezea hukumu za Allah, na kwa waliyoyaharamisha na kuhalalisha kwa utashi wao, na kwa dhuluma walizozifanya, lakini tunaa-shiria ujinga wao dhidi ya hukumu za Allah na dini, na mfano wa watu kama hawa waliowajinga, wapuuzi na waongo hawawezi kufikia daraja za maimamu au kuwa ni viongozi wa umma”¹

“Hakika amali za Omar ni zenye kutokana na chimbuko la kufuru, uzandiki na kwenda kinyume na aya zilivyokuja katika Quran”².

Maoni “Amebakisha kitu gani Khomeni kwa wafuasi wake kukisema? Ikiwa kiongozi mkuu na marejeo makuu na muasisi wa mapinduzi ni mwenye ulimi mchafu na kuongoza kwa matusi na kutukana masahaba, jee wafuasi watakuwa hali gani?, haya wayaone wale wanaolingania ukaribu na umoja. Mwenye maneno haya ndie mwenye wito wa siku ya kimataifa kwa ajili ya Al-qudusi na juma la umoja wa waislam, Pole pole enyi walinganiaji wa ukaribu na umoja).

19- Alkhomeiny anasema: Hakika waislamu huko akhera hawatopata fadhila na rehema za Allah, hizo ni kwa ajili ya Shia tu peke yao!

Amenukuu Alkhomeiny hadithi kutoka kwa Swaduuq:
﴿فَأُولَٰئِكَ يَدُلُّ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۖ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا﴾ [الفرقان: ٧٠]
"Hao ndio Allah anaobadilisha mabaya yao kuwa mema, na Allah ni msamehevu na mwenye kurehemu), kasema (as):
“Ataletwa muumin mwenye madhambi siku ya kiyama atasima-mishwa uwanja wa hisabu, Allah atakuwa ndie mwenye kumu-hisabu, hakuta kuwa na mtu yeyote atakaejua, atamtambulisha madhambi yake, atakapokiri makosa yake Allah huwaambia waandishi: Yabadilisheni yawe ni mema na yatokezeni kwa watu,

¹ Kashfu al-asrari uk, 107-108
² Kashfu al-asrari, 116

hapo watu watasema: Mja huyu hakuwa na kosa hata moja! Kisha Allah ataamuru apelekwe peponi, hii ndio tafsiri ya aya, na hii ni kwa wenye madhambi katika mashia wetu tu”. Alkhomeiny kaitolea maelezo riwaya hii akasema:

"Inajuilikana kwamba jambo hili ni la shia wa Ahlul bayt tu, watu wengine haliwahusu. Kwa sababu imani haipatikani isipokua kwa njia ya wilaya (uongozi) wa Aliy na mawasii wake (maimamu baada yake) watoharifu walioepushwa na madhambi (as), bali imani ya kumuamini Allah na Mjumbe wake haikubaliwi bila ya kuamini wilaya (uongozi) kama tutakavyotaja hayo katika mlango unaofuata".¹

20- Alkhomeiny anasema: Watu wa Irani ni bora kuliko watu wa Hijaz katika zama za Mtume (saw):

"Mimi nina dai kwa kujiamini kwamba watu wa Irani kwa mamilioni yao zama hizi za sasa ni bora kuliko watu wa Hijaz katika zama za Mtume ﷺ, na ni bora kuliko watu wa Kuufa huko Iraq katika zama za Amiril Muuminin na Al Husain ibni Aliy (as). Watu wa Iraq na wa Kuufa walifanya muamla mbaya sana na Amiril Muuminin na wakamuasi, na malalamiko ya Imam dhidi yao yanajuilikana katika vitabu vya historia na tarekh, na waislamu wa Iraq na wa Kuufa wamefanya waliyoyafanya kwa Sayyid Shuhadaa (Alhusain ibnu Aliy), hao ni wale wasiotenda dhambi ya kumuua, wakawa ima wamekimbia vita au wamekaa mpaka yakatokea mauaji hayo ya kihistoria".²

Angalizo: (Kama Khomeini angalikuwa yuko hai akaona maandamano ya mamilioni -ya kizazi cha watoto wakimapinduzi waliosoma mitaala yake- wanakanyagakanyaga picha zake na kuzitia moto, jee angaliwasifia kwa sifa kama hizo? au angaliwaita nawaasib (maadui wa Aalil Bait) na ni wafuasi wa umawiyiina na abasiyiina?

21-Khomeini anajawizisha kuingiliwa mwanamke kwa nyuma (kwenye duburi).

"Masuala ya kumi na moja; ni mashuhuri na yenye nguvu kuwa kumuingilia mtu mkewe kwa nyuma ni yenye kujuzu, japo ni karaha na kuacha ni bora zaidi, hasa ikiwa hakuna ridhaa ya mwanamke.

Masuala ya kumi na mbili: Haijuzu kumuingilia mwanamke kabla ya kufikia miaka tisa, ni sawa kama ni ndoa ya kudumu au ni ya muda, ama mambo mengine ya kustarehe nae kwa kumpapasa kwa ajili ya matamanio na kumkumbatia na kumuweka mapajani, hakuna kosa kwa hilo hata akiwa ni mwenye kunyonya"³

¹ Al-arbauna hadithi lilkhomeyni, 511
² Alwasiya alsiyasiya al-ilahiya lil-imam alkhomeyni, uk 27
³ Tahriri al-wasila, uk 221

Angalizo: (Uchafu wa mtu huyu umekiuka mipaka, na katika itikadi zake ni mtu wa khurafati amechupa mipaka na mwenye chuki na katika fiqhi ya jinsi, ni wenye kujawizisha na kuwepe-sisha kila kitu, usishangae huyu ndiye Khomeini kiongozi wa mapinduzi mapotofu.

22-Khomeini anatoa fatwa ya kuhalalisha kuchukuliwa mali ya muislam sunni, na kwamba sunni ni najisi wala haipaswi kusaliwa (jeneza lake).

"Naam itakubalika endapo itakuwa si unyang’anyi kutoka kwa muislam au dhimy au mwenye kuishi kwa mkataba au mwengineo katika watu ambao mali zao zinaheshimika. Na kauli yenye nguvu ni kwamba naaswiby huunganishwa na makafiri wapiga vita kuhusu kujuzu ngawira zilizopatikana kutoka kwao na kwamba zinawajibikiwa na khumusi bali inaonyesha kwamba inajuzu kuchukuwa mali yake popote pale na kwa njia yoyote".¹

"Na wala haijuzu kumsalia kafiri wa aina yoyote, hata akiwa ni murtadi na atakaehukumiwa kufuru, katika wale wanaodai uislam mfano wa nawaasib (masunni) na khawaarij"²

"Na nawaasib na Khawaarij wote ni najis bila ya shaka yoyote".³

Angalizo: (hakuna shaka kwamba makusudio ya alnawasib hapa ni ahlusunna, masahaba na maimamu wanne wote na Bukhari na Muslim na maulamaa wengine wa kiislam, cha kuzingatia hapa ni kupambanua kwake baina al-nawaasib na kahawaarij kwa kuwafanya ni makundi mawili, hii ina maana kwamba al-nawasib siyo alkhawarij, na wasio alkhawarij sio wengine ila ni ahlusuna, na tuzingatie hili wenye akili!).

23- Khomeini anasema kuweka mkono wakulia juu ya kushoto kwenye sala kunaibatilisha sala.

"Jambo la pili lenye kubatilisha sala, kukufuru, nako ni kuweka mkono juu ya mkono mwengine kama wanavyofanya watu wengine wasio sisi, na kwa kauli yenye nguvu kufanya hivyo kunabatilisha sala akifanya kwa makusudi, siyo kwa kusahau, na vizuri zaidi ni kuirejea sala hiyo, na ataruhusiwa kufunga mikono kama atafanya kwa taqiyya"⁴.

24-Khomeini anawahimiza askari wa kikosi cha walinzi wa mapinduzi wa Jamhuri ya Irani kuwauwa mahujaji wa nyumba tukufu ya Makka mwaka 1407 hijria

Tarehe sita dhulhijah mwaka 1407 hijria, ilikuwa ni siku ya

¹ Tahriri al-wasila, uk 1/80

² Tahriri al-wasila, uk 1/80

³ Tahriri al-wasila, uk 1/80

⁴ Tahriri al-wasila, uk 166

mtihani mkubwa ulioutikisa ulimwengu, msimamizi mkuu wa fitina hii na mchochezi wake ni Khomeini mchamungu mwana ibada, aliyefanya kila hima kuhakikisha inatokea, licha ya majaribio kadhaa ya kuuzima moto wa fitina hiyo. Ulimwengu umewashuhudia askari wa kikosi cha walinzi wa mapinduzi wa Iran waliovaa nguo za mahujaji (ihram), wakivunya utakatifu wa ardhi tukufu na kusababisha fitna ambayo imeacha mamia ya wafu na maelfu kujeruhiwa miongoni mwa mahujaji. Fitna hii ilianza kwa maandamano ambayo yalijionyesha pale awali kama ni ya amani lakini baadae yakageuka, waandamanaji wakaonekana wakiwa wamebeba visu, mapanga, vitu vyenye ncha kali na petrol huku wakinyanyua picha za Alkhomeiny muanzilishi wa fitna hii na mchochezi wake.

Angalizo: (Mwenye kutambua itikadi za Khomeini na chuki zake dhidi ya ardhi tukufu, atatambuwa kiwango cha uadui wake, Khomeni ni kioingozi ni marejeo na waliyul faqiyh wa dola linalofikiriwa kuheshimu sheria, anafanya ugaidi kama unavyofanywa na wanamgambo wa makundi yenye silaha yaliyo nje ya sheria. Kwa kweli Khomeiny hapa amefanya kama alivyofanya Abraha wa Habasha, na kwa hivyo Alkhomeiny sio waliyul Faqiih bali ni Abraha Mpuuzi).

25-Khomeini ni marejeo ya asili katika vazi la udikteta

Khomeini ametumia njia nyingi za mauaji na vitisho kwa wapinzani wake, kwa hoja kwamba yeye ni kivuli cha Allah ardhini, akaibadilisha Iran kuwa ni mahakama ya upekuzi (upelelezi), kwa kupekua nia za watu na kuwahukumu, akawaweka viongozi wa ahlu sunna katika vizuizi vya nyumbani na kuwazuilia aina zote za harakati za kidaawa, au hata za kisiasa, bali akafikia kuzuia wasijenge hata misikiti katika mji wa Teheran, ilifikia chuki yake kumtia ndani Mufti Sheikh Ahmad Zaadah mpaka kufa kwake. Wakati akiwakanadamiza ahlusunna upande mwingine alikuwa mwepesi kwa mayahudi na manasara, na akawajengea masinagogi na makanisa wala hakuyazuia. Haya ndiyo yaliyokuwa yakitendeka ndani, ama nje kwa kutumia kauli mbiu za uongo, alizokuwa akizipeperusha kama kuwanusuru wanyonge na kuwalinda waislam, alikuwa akifanya mikataba ya manunuzi ya silaha kwa Wamarekani na Israel, na fedheha ijulikanayo kwa -Iran gate- ni ushahidi tosha dhidi yake na serikali yake, nyongeza ya hayo ni kusalimu kwake amri mbele ya jeshi la Iraq ambalo lilisonga mbele kila upande wala haukumfalia kitu wito wa kisasi cha Husein wa maombi yake kwa Mahdi wake anaedai.

Kwa kupata mengi zaidi kuhusu uhakika wa Alkhomeiny tembelea mtandao wa Al Imam Alkhomeiny:

<http://www.khomainy.com>